Epuka Kujitakia Makuu!

Maagizo: Fanya zoezi hili katika mazingira matulivu. Unaposoma maandiko, jiwazie ukiwa katika matukio yanayozungumziwa. Wazia kikao. Sikia sauti. Hisi kama wahusika wanavyohisi. Wazia kwamba masimulizi haya ni halisi kabisa.

Wahusika Wakuu: Daudi, Absalomu, Yoabu

Muhtasari: Absalomu ajaribu kupindua ufalme wa baba yake.

❶ ***CHUNGUZA TUKIO HILI.—SOMA 2 SAMWELI 14:25-33; 15:1-17; 18:9-17, 30-33.***

Eleza jinsi Absalomu alivyoonekana, kama unavyomwazia. (*Soma tena 2 Samweli 14:25, 26.*) _____

_____

Unawazia sauti na mtazamo wa Absalomu ulikuwaje alipokuwa akishawishi mioyo ya watu waliokuja kwa mfalme kutafuta haki? (*Soma tena 2 Samweli 15:2-6.*)

_____

Unatambua nini kuhusu utu wa Absalomu kutokana na tukio lililoandikwa kwenye 2 Samweli 14:28-30? _____

_____

❷ ***CHIMBA ZAIDI.***

Absalomu alikuwa amefanya mpango gani ili kunyakua ufalme? (*Dokezo: Soma 2 Samweli 13:28, 29. Amnoni alikuwa mwana mzaliwa wa kwanza wa Daudi na hivyo angerithi kiti cha ufalme.*) _____

_____

Ingawa alikuwa na tamaa ya kupata makuu na alijaribu kujitafutia sifa, jinsi Absalomu alivyozikwa inaonyesha nini kuhusu vile ambavyo kwa kweli watu walimwona?- (*Soma tena 2 Samweli 18:17.*) _____

_____

Unafikiri ni nini kilichochangia Absalomu awe na roho ya kujitakia makuu? (*Kwa kulinganisha, soma maelezo kuhusu Diotrefe kwenye 3 Yohana 9, 10.*) _____

_____

Daudi aliathiriwaje na matendo ya Absalomu? (*Dokezo: Soma Zaburi ya 3, ambayo Daudi aliiandika wakati wa uasi wa Absalomu.*) _____

_____

_____

3 *TUMIA MAMBO ULIYOJIFUNZA. ANDIKA MAMBO ULIYOJIFUNZA KUHUSU . . .*

Hatari ya kujitakia makuu. _____

_____

Maumivu ambayo mtu anaweza kuwasababishia wengine, kutia ndani wazazi wake, kwa sababu ya matendo yake. _____

_____

NJIA NYINGINE UNAYOWEZA KUTUMIA HABARI HIYO.

Unawezaje kunaswa na mtego wa kujitakia makuu? _____

_____

Unawezaje kuepuka kusitawisha kiburi?

_____

_____

4 *NI MAMBO GANI KATIKA SIMULIZI HILI AMBAYO YAMEKUGUSA MOYO SANA, NA KWA NINI?*

_____

_____

Mapendekezo: Wazia matokeo yangekuwaje ikiwa Absalomu angetenda ifaavyo. Ni nini ambacho kingetokea ikiwa Absalomu angekuwa mwenye kiasi badala ya kujitakia makuu?—Methali 18:12.

www.jw.org © 2012 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania